**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**

# MWONGOZO WA HUDUMA KWA WATUMISHI WA UMMA WENYE ULEMAVU

**Ofisi ya Rais,**
**Menejimenti ya Utumishi wa Umma,**
**Dar es Salaam.**

## YALIYOMO

Ukurasa


i. **Dibaji** … … … … … … …

**Sura ya Kwanza: Fasili/Ufafanuzi na Taratibu za Kisheria** …
1.1 Madhumuni ya Mwongozo … … … … …
1.2 Nani atatumia mwongozo? … … … … … …

**Sura ya Pili: Hali Halisi ya Watu wenye Ulemavu Tanzania** …
2.1 Watu wenye Ulemavu katika Utumishi wa Umma … … …

**Sura ya Tatu: Kanuni za kufuata ili kuwapa watu wenye ulemavu uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi na uadilifu wenye ulemavu**
3.1 Kukuza uelewa … … … … … … … …
3.2 Utunzaji wa siri … … … … … … … …
3.3 Kuondoa ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu … … … …
3.4 Usumbufu/Bughudha … … … … … … …
3.5 Kutoa haki na fursa sawa … … … … … … …
3.6 Fursa ya kuyafika na kuyatumia majengo ya ofisi … …
3.7 Upatikanaji wa taarifa na mawasiliano … … … …
3.8 Usawa wa Kijinsia na Ulemavu … … … … …
3.9 Kuwalinda Watu wenye Ulemavu dhidi ya maambukizo ya UKIMWI …
3.10 Huduma za Afya
3.11 Kuwezesha watu wenye ulemavu kuishi maisha ya kawaida … …
3.12 Nyenzo na vifaa vya kuwaongezea uwezo wenye ulemavu …
3.13 Mabadiliko ya lazima ya kazi … … … … … …
3.14 Matunzo na Misaada ya kujimudu … … … … … …
3.15 Usafiri na usalama barabarani … … … … … …

**Sura ya Nne: Kuajiri na Kudumisha Kazini Watu wenye ulemavu**
4.1 Matangazo ya kazi … … … … … … …
4.2 Usaili/Mahojiano … … … … … …
4.3 Mafunzo … … … … … … … … …
4.4 Malalamiko na Taratibu za Kinidhamu … … … …
4.5 Masharti ya Huduma … … … … … … …
4.6 Kushughulikia kazi za ziada … … … … … …
4.7 Likizo ya Ugonjwa … … … … … … …

**Sura ya Tano: Kuandaa Mipango** … … … … …
5.1 Hatua za kufuata kabla ya kuanza kuandaa mipango … …
5.2 Kukusanya taarifa kwa ajili ya mchakato wa kuandaa mipango …

5.3 Kupanga Bajeti … … … … … … …

**Sura ya Sita: Haki na Wajibu** … … … … …
6.1 Waajiri na Ajira katika Utumishi wa Umma … … …
6.2 Watumishi wenye Ulemavu … … … … … …

# DIBAJI

Mwongozo huu unatoa maelekezo ya namna ya kuboresha mazingira ya ajira na kazi kwa watu wenye ulemavu ndani ya utumishi wa umma, wanapokuwa kazini au wanapoomba kazi. Mwongozo unaeleza juu wajibu wa taasisi za serikali katika kuwahudumia watu wenye ulemavu na kuwasaidia kudai haki zao pindi wanapobaini kwamba wamebaguliwa.

Mwongozo unazihimiza Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuwa mfano wa kuigwa katika kuwatendea haki watu wenye ulemavu. Ni vyema kukumbuka kwamba mapungufu ya kiutendaji waliyonayo watu wenye ulemavu hayawezi kuwafanya wasiwe na uwezo wa kushiriki katika shughuli za kijamii. Mara nyingi sababu za kimazingira, kama vile namna ofisi ilivyojengwa au taratibu za kiutendaji, ndizo zinazoathiri ushiriki wa watu wenye ulemavu katika shughuli za kijamii.

Mlemavu ni mtu mwenye udhaifu wa kimwili na kiakili ambao unaathiri uwezo wa kufanya kazi zake za kila siku. Athari au udhaifu huo hauna budi kuwa mkubwa, mbaya na wenye athari kubwa au wa muda mrefu, yaani muda usiopungua mwezi mmoja au wa maisha yake yote.

Shirika la Afya Duniani linakadiria kuwa katika kila jumuia, asillimia kumi (10%) ya watu wake wana aina fulani ya ulemavu wa kimwili na kiakili. Nchini Tanzania inakadiriwa kuwa watu milioni tatu (3,000,000) kati ya watu zaidi ya milioni thelathini (30,000,000) wana ulemavu wa aina mbalimbali. Pamoja na juhudi nyingi zinazofanywa na serikali kuongeza idadi ya watu wenye ulemavu katika Utumishi wa umma, idadi yao bado ni ndogo kwa vile kuna idadi ndogo ya watu wenye ulemavu wenye elimu ya kutosha. Hali hii inatokana na uwiano mdogo wa watoto wenye ulemavu ambao wanapata elimu katika ngazi zote.

Serikali inachukua hatua mbalimbali ili kuboresha mazingira ya kazi kwa watu wenye ulemavu katika utumishi wa umma. Hatua hizi ni pamoja na kutunga Sheria, Sera, Miongozo na kuandaa mazingira mazuri ya wadau mbalimbali kushiriki katika kutatua matatizo wanayokumbana nayo watu wenye ulemavu.

Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma Kwa Watu Wenye Ulemavu (National Disability Policy) iliyoidhinishwa na Baraza la Mawaziri mwezi Julai, 2004 inasisitiza kuhusu utoaji wa fursa sawa kwa watu wenye ulemavu. Kauli mbiu katika sera hii ni Maendeleo na watu wenye ulemavu, huduma bora kutolewa kwa kuzingatia usawa, na usawa kwa wenye ulemavu. Sera hii inahimiza pia

kuhusu ushiriki wa watu wenye ulemavu katika maendeleo ya nchi hususan katika mipango ya kupunguza umaskini katika ngazi zote.

Sera na Sheria mbambali zinazohusu watu wenye ulemavu zitasaidia kuboresha fursa za ajira, kupiga vita ubaguzi, na kuwawezesha watu wenye ulemavu kuishi maisha yenye hadhi. Aidha, Sera na Sheria hizi zitawawezesha watu wenye ulemavu kushiriki katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Licha ya juhudi hizi za kutunga Sheria na kutoa Sera, utekelezaji wake unategemea uwepo wa mfumo ambao unampa kila mdau wajibu wa kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu katika sekta yake. Nina imani kwamba matokeo ya utekelezaji wa Mwongozo huu yatazingatia mawazo ya kila mdau ili kufanikisha adhima iliyokusudiwa na kuleta ufanisi katika utumishi wa umma. Kwa hiyo, umuhimu wa Mwongozo huu umekuja wakati muafaka.

George Yambesi
**Katibu Mkuu**
**Ofisi ya Rais,**
**Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

# SURA YA KWANZA

# FASILI/UFAFANUZI NA TARATIBU ZA KISHERIA

## Utangulizi

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatambua umuhimu wa suala la kuboresha mazingira ya kazi na ajira kwa watumishi wa umma wenye ulemavu mahali pa kazi. Mwongozo huu ni kanuni ambayo Wizara, Idara na Mawakala wa Serikali watatumia kama dira yao katika kuwahudumia watumishi wa umma wenye ulemavu mahali pa kazi.

Mwaka 2005, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilifanya utafiti juu ya Menejimenti Anuai ya Jamii (Diversity Management) katika Utumishi wa Umma. Utafiti huu ulionyesha, pamoja na mambo mengine, kwamba mojawapo ya masuala ya anuai za jamii katika Utumishi wa Umma nchini Tanzania ni watu wenye ulemavu.

Mwongozo wa kushughulikia Watumishi wa Umma wenye Ulemavu Mahali pa Kazi unatolewa kama nyenzo ambayo ni rahisi kuitumia wakati wa kuandaa mipango, utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini ya mipango mbalimbali inayohusu watumishi wenye ulemavu katika utumishi wa umma. Mwongozo huu utafafanua kanuni na maelekezo muhimu, matumizi ya sheria zilizopo, taratibu za utekelezaji, mipango na bajeti kwa ajili ya huduma kwa watumishi wa umma wenye ulemavu.

## 1.1 Madhumuni ya Mwongozo

Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu utakuwa na madhumuni yafuatayo:

- Kuuwezesha Utumishi wa Umma kuwahudumia ipasavyo watu wenye ulemavu na kuleta haki na fursa sawa kwa wote mahali pa kazi;
- Kushughulikia masuala ya usawa na kuhamasisha watumishi wa umma waweze kutambua matatizo waliyonayo watumishi wenye ulemavu mahali pa kazi;
- Kupendekeza utekelezaji wa mikakati ambayo itaboresha fursa za ajira kwa watu wenye ulemavu;
- Kuimarisha uwezo wa kutekeleza ipasavyo Sheria zinazohusu ajira kwa watu wenye ulemavu;

- Kurahisisha taratibu za ajira kwa watu wenye ulemavu wanapoomba kazi.

Madhumuni makuu ya mwongozo huu ni:

(i) Kuleta haki na usawa wa fursa mahali pa kazi;
(ii) Kukiwezesha kitengo cha Anuai za Jamii katika Ofisi ya Rais, menejimenti ya Utumishi wa Umma kuandaa mpango wa utekelezaji wa masuala ya watu wenye ulemavu katika Utumishi wa Umma.

## 1.2 Nani atatumia Mwongozo huu?

Mwongozo huu utatumiwa na waajiri na watumishi wote katika utumishi wa umma. Wadau wakuu ni:-

(i) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.
(ii) Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana;
(iii) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto;
(iv) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi;
(v) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii;
(vi) Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
(vii) Ofisi ya Mwakilishi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO);
(viii) Watumishi wenye ulemavu wanaofanya kazi katika utumishi wa umma;
(ix) Vyama na taasisi zote zinazojishughulisha na masuala ya watu wenye ulemavu.

Mwongozo huu utasomwa pamoja na Sheria, Sera na Kanuni mbalimbali za Utumishi wa Umma kama ifuatavyo:

(i) Sheria ya Ajira kwa Watu Wenye Ulemavu Na. 2 ya mwaka 1982.
(ii) Tangazo la Serikali Na. 464 kuhusu Kanuni za Ajira kwa Watu Wenye Ulemavu la Mwaka 1985.
(iii) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Na. 5 ya Mwaka 1978;
(iv) Sera ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004;
(v) Sera ya Menejimenti na Ajira Katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 1999.

(vi) Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma (Standing Orders), 1994,
(vii) Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003

## SURA YA PILI.

## HALI HALISI YA WATU WENYE ULEMAVU NCHINI TANZANIA.

### Utangulizi

Kutokana na kukosekana kwa takwimu za idadi ya watu wenye ulemavu katika takwimu za sensa iliyofanyika mwaka 2002, idadi ya wenye ulemavu nchini Tanzania inaweza kukadiriwa kutumia vigezo mbalimbali. Shirika la Afya Duniani (ILO), kwa mfano, linakadiria kwamba asilimia kumi (10%) ya watu katika kundi lolote la jumuia wana ulemavu wa aina fulani. Kwa hiyo, Tanzania yenye idadi ya watu milioni 34.4 (kwa mujibu wa sensa ya watu ya mwaka 2002), inakadiriwa kuwa na watu milioni 3.4 wenye ulemavu wa aina mbalimbali kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 1: Takwimu za watu wenye ulemavu Tanzania.**

| | |
|---|---|
| ▪ Ulemavu wa viungo … … … … … | 967,932 |
| ▪ Wasioona … … … … … …. … | 933,363 |
| ▪ Wasiosikia … … … … … … … | 691,380 |
| ▪ Ulemavu wa kiakili … … … … … | 276,552 |
| ▪ Ulemavu mchanganyiko … ... … … … | 138,276 |
| ▪ Ulemavu wa aina nyingine (Usiojulikana) … … | 449,397 |
| **JUMLA** | **3,456,900** |

Watu wenye ulemavu nchini Tanzania wanakabiliana na changamoto nyingi katika maisha yao ya kila siku. Vikwazo vya kiuchumi ambavyo vilisababishwa, pamoja na mambo mengine, na tatizo la madeni na utandawazi, vimeathiri sana maisha ya watu wenye ulemavu. Utoaji wa huduma za afya, elimu, mafunzo ya stadi, ajira na misaada ya kiufundi kwa watu wenye ulemavu umezidi kupungua.

Kutokana na uwezo mdogo wa kupata mahitaji ya msingi walionao, watu wenye ulemavu wamejikuta wakikabiliwa na matatizo mbalimbali katika

jamii. Matokeo ya hali hii ni kupungua kwa ushiriki wao katika masuala mengi ya kijamii. Ifuatayo ni mifano ya mambo yanayowapata watu wenye ulemavu nchini Tanzania:

- Kuna uhusiano mkubwa kati ya ulemavu na umaskini ambao unakuzwa zaidi kutokana na kukosa fursa ya kupata elimu;
- Watu wenye ulemavu ni miongoni mwa wananchi walio na umaskini zaidi;
- Watu wenye ulemavu wako katika hatari zaidi ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Kwa mfano, asiyesikia hataweza kusikia matangazo yanayotolewa redioni au kwenye televisheni juu ya kujikinga na maambukizo ya Virusi vya Ukimwi na UKIMWI na athari zake. Vilevile mtu asiyeona hataweza kusoma machapisho mbalimbali yanayohusu kujikinga na maambukizo ya Virusi vya Ukimwi na kuenea kwa UKIMWI na athari zake. Pia hataweza kupambanua matumizi salama na uimara wa kondom.

## 2.1 Watu Wenye Ulemavu Katika Utumishi wa Umma.

Idadi ya watumishi wa umma wenye ulemavu bado ni ndogo ukilinganisha na wingi wao katika jamii. Utafiti wa Masuala ya Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma nchini Tanzania uliofanywa na taasisi ya Enst and Young mwaka 2005 ulibainisha kuwa idadi ya watumishi wenye ulemavu ni chini ya asilimia moja (1%) ya watumishi wote wa umma. Aidha, kwa mujibu wa taarifa za watumishi wenye ulemavu zilizokusanywa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma mwezi Julai hadi Desemba 2007, jumla ya watumishi 689 au asilimia 0.2 ya watumishi wote wa umma 354,000, waliorodheshwa kuwa na ulemavu wa aina mbalimbali.

Taarifa hizi zinaonesha kuwa ipo haja ya kulinda, kuboresha na kurahisisha ushiriki wa watu wenye ulemavu katika ajira ya umma. Serikali ya Tanzania imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kuongeza nafasi za ajira kwa watu wenye ulemavu katika utumishi wa umma.

Tafiti mbalimbali zilizofanywa zinaonyesha kwamba ipo haja kwa serikali kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi na bila matatizo pale wanapopata ajira. Kwa mfano, Utafiti wa “Menejimenti ya Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma” iliofanywa na Taaisisi ya Ernst and Young Mwaka 2005, ulibaini mambo yafuatayo:

- Kuna umuhimu wa kukusanya na kutunza takwimu za watu wenye ulemavu katika utumishi wa umma;

- Kuna umuhimu wa kutenga nafasi za kazi maalum kwa watu wenye ulemavu katika utumishi wa umma;
- Kuna umuhimu wa kutoa na kuimarisha huduma kwa watu wenye ulemavu katika Utumishi wa umma;
- Kuna umuhimu wa kuweka mipango ya usafiri wa kwenda na kurudi kazini kwa watumishi wenye ulemavu hasa mijini.

# SURA YA TATU

## KANUNI ZA KUFUATA ILI KUWAPA UWEZO WA KUFANYA KAZI KWA UFANISI WATUMISHI WENYE ULEMAVU

### Utangulizi

Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zichukue hatua mahsusi za kuwaelimisha watumishi wote juu ya watu wenye ulemavu, haki zao, mahitaji yao, uwezo wao na mchango wao katika utendaji wa kazi katika utumishi wa umma. Ili kufikia lengo hili kanuni zifatazo zitafuatwa:-

### 3.1 Kukuza Uelewa.

(a) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zisambaze taarifa mpya juu ya programu na huduma zilizopo kwa watumishi wenye ulemavu, familia zao, wataalamu wa masuala ya ulemavu na umma kwa jumla. Taarifa kwa watu wenye ulemavu zitolewe katika njia itakayowarahisishia kupata taarifa iliyokusudiwa. Kwa mfano, kwa kutumia maandishi yenye nukta nundu (blaille) kwa wasioona na kwa kutumia lugha ya alama kwa viziwi nk.

(b) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinahimizwa kuanzisha kampeni za utoaji habari kupitia vyombo mbalimbali (redio, televisheni, magazeti na intaneti) juu ya Sera ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004, na pia kusisitiza kwamba watu wenye ulemavu ni sawa na raia wengine, hivyo wanastahili kupata haki zao za msingi na pia wanawajibika kwa taifa. Elimu kama hii itahalalisha mipango

inayopangwa ya kuwapa uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii.

(c) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihimize utoaji wa taarifa sahihi juu ya watu wenye ulemavu katika vyombo vya habari. Watumishi wenye ulemavu na Maafisa wa Vitengo vya Habari na Mawasiliano washirikishwe ipasavyo katika kuamua aina ya ujumbe na taarifa zinayofaa kutolewa katika vyombo vya habari.

(d) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itayarishe programu za elimu kwa umma ambazo zitaonyesha Kanuni za ushiriki kamilifu wa watu wenye ulemavu katika shughuli za kijamii pamoja na watu wenye ulemavu kupata haki sawa.

(e) Wizara, Idara, Mawakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwaalike watumishi wenye ulemavu na familia zao kushiriki katika programu za elimu kwa jamii kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu.

(f) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zianzishe na kukuza programu zenye lengo la kutoa uelewa kwa watu wenye ulemavu juu ya haki zao na uwezo walionao wa kufanya kazi.

(g) Programu za kukuza uelewa wa masuala ya ulemavu zitakuwa sehemu muhimu ya elimu kwa watumishi wenye ulemavu na familia zao ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali katika jamii. Watumishi wenye ulemavu wasaidiane wao kwa wao katika kukuza uelewa kwa kupitia shughuli za vyama vyao na wanaharakati wa haki za binadamu.

## 3.2 Utunzaji wa Siri.

(a) Watu wenye ulemavu wasilazimishwe kutoa hadharani taarifa za kidaktari kuhusu ulemavu wao na wanaweza kutoa taarifa hizo kwa Maafisa husika tu ili waweze kupewa huduma maalum.

(b) Maafisa husika Utumishi wa Umma watunze taarifa za siri za watu wenye ulemavu kwa namna ambayo haziwezi kuonekana na mtu ambaye hahusiki. Utaratibu huu utaondoa udhalilishaji na dharau kwa watu wenye ulemavu katika jamii.

(c) Vielelezo au hati za matibabu vinavyotolewa ili mtumishi mwenye ulemavu aweze kupewa huduma maalum vitolewe kwa maafisa wanaohusika tu.Vielelezo au hati hizo zihifadhiwe katika jalada la siri la mtumishi mwenye ulemavu na sio kwenye jalada lake la wazi.

### 3.3 Kuondoa ubaguzi dhidi ya Watu wenye ulemavu

Ubaguzi na dharau kwa watumishi wenye ulemavu kunaweza kuondoa ustawi wa watumishi wenye ulemavu na mazingira mazuri ya kazi. Ni wajibu kwa kila mwajiri kuhakikisha kuwa watumishi wenye ulemavu hawabaguliwi au kubudhudhiwa katika maeneo ya kazi. Kwa hiyo:-

(a) Sheria, Kanuni, Sera na Miongozo ya Utumishi wa Umma zinayokataza na kukemea ubaguzi na unyanyasaji dhidi ya watumishi (ikiwa ni pamoja na watumishi wenye ulemavu) zisimamiwe na kutekelezwa kikamilifu. Watumishi wenye ulemavu wasinyanyaswe au kubaguliwa kwa misingi ya ulemavu halisi au wa hisia utakaofanywa kuhusiana na maombi ya kazi, ajira, kupata vifaa maalumu, fidia, mafunzo au malipo yanayotokana na utumishi wao;

(b) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwalinde watumishi wenye ulemavu dhidi ya aina yoyote ya dharau; ubaguzi, uonevu na usumbufu kutoka kwa wafanyakazi wengine. Hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa mtumishi yeyote atakayetenda vitendo hivi kwa watumishi wenye ulemavu;

(c) Mtumishi mwenye ulemavu asiachishwe kazi au kukataliwa kubadilishiwa kazi pale inapoonekana wazi kwamba hawezi kumudu kufanya kazi yake ya awali kutokana na ulemavu alionao;

(d) Mtumishi mwenye ulemavu anapokuwa na uwezo wa kutekeleza wajibu wake wa kazi, apewe haki ya kufanya hivyo na pia apewe fursa na haki zingine zinazoendana na kazi yake kama watumishi wengine;

(e) Mtu mwenye ulemavu anapofanyiwa upendeleo chanya, kwa mfano, kumnunulia vifaa na nyenzo za kujimudu, isieleweke kama ni upendeleo bali ni haki inayotokana na yeye kuwa mwenye ulemavu.

**Jedwali Na. 2: Mifano ya ubaguzi kwa wenyeUlemavu.**

| |
|---|
| ▪ Kumnyima mtumishi mwenye ulemavu ajira, huduma au nyumba kwa sababu ya ulemavu wake.<br><br>▪ Kumtendea tofauti na wengine, kumtenga au kupendelea (bila sababu maalum) kwa sababu ya kuwa na hali tofauti na wengine.<br><br>▪ Kukataa kumpa au kutompa kwa makusudi mwenye ulemavu, fursa ya ajira (Isipokuwa katika nafasi au kazi ambazo hawezi kumudu kwa sababu ya hali yake) ambayo inampa nafasi ya kupandishwa cheo, uhamisho, mafunzo au kupokea manufaa mengine. |

## 3.4 Usumbufu/Bughudha.

(a) Usumbufu hutokea mahali ambapo, kwa sababu ya hali ya ulemavu wa mtumishi, mtu mwingine anafanya vitendo vyenye lengo la:-

(i) Kuvunja hadhi ya utu wake;
(ii) Kuleta mazingira ya vitisho, uadui, uhasama, kumvunjia heshima, kuaibisha na uchokozi.

(b) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa watumishi wote wanafahamu maana na athari za usumbufu kwa mtumishi mwenye ulemavu. Taarifa za kuelimisha watumishi zitolewe kwa kutumia njia mbalimbali kama vile mabango, vipeperushi, programu za redio na televisheni au zibandikwe kwenye mbao za matangazo.

(c) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihamasishe watumishi kutoa taarifa za vitendo vyovyote vya usumbufu wanavyotendewa wenye ulemavu mahali pa kazi. Taarifa hizi zitolewe kwa mdomo au maandishi kwa Maafisa husika au kwa kupitia katika visanduku vya maoni. Waajiri wahakikishe kuwa mashauri ya aina hii yanashughulikiwa kikamilifu na hatua za kinidhamu zinachukuliwa dhidi ya wakosaji.

## 3.5 Utoaji wa haki na fursa sawa.

Kutoa haki na fursa sawa ni mchakato ambao mifumo mbalimbali ya jamii na huduma hutolewa kwa watu wote bila ubaguzi. Kanuni ya haki na fursa sawa kwa wote inatambua kwamba mahitaji ya kila mmoja yana

umuhimu unaolingana. Mahitaji hayo ndiyo msingi katika kupanga mipango ya maendeleo ya watumishi na kwamba rasilimali iliyopo inapaswa kutumika kwa namna ambayo kila mmoja atapata haki na fursa sawa ya kushiriki.

(a) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kutambua kwamba watumishi wenye ulemavu wana haki na wajibu sawa kama watumishi wengine mahali pa kazi. Kwa hiyo, wanapaswa kupata huduma wanazohitaji (Afya, Elimu na huduma nyingine za kijamii) katika mfumo na utaratibu wa kawaida.

(b) Kama sehemu ya mchakato wa kutoa haki na fursa sawa kwa wote, waajiri waweke utaratibu wa kuwasaidia watumishi wenye ulemavu kutekeleza wajibu wao kikamilifu katika sehemu za kazi kama watumishi wengine.

## 3.6 Fursa ya kuyafikia na kuyatumia majengo ya ofisi

Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zifanye marekebisho ya miundombinu iliyopo ikiwa ni pamoja na majengo ili yaweze kutumiwa kwa urahisi na watumishi wote, ikiwa ni pamoja na watumishi wenye ulemavu. Baadhi ya marekebisho hayo ni pamoja na kuweka sehemu maalum za maegesho, vyoo, ngazi (ramps) na samani nyingine maalum kwa ajili ya watumishi wenye ulemavu.

(a) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika, zihakikishe kwamba wajenzi, wahandisi na wataalamu wengine wa ujenzi wa nyumba wana uelewa wa kutosha juu ya Sera ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004 pamoja na Mwongozo huu ili waweze kuchukua hatua zinazofaa wakati wa ujenzi wa majengo ya ofisi za serikali.

(b) Mamlaka zinazohusika na masuala ya ujenzi zihakikishe kuwa mahitaji ya watu wenye ulemavu yanazingatiwa kikamilifu wakati wa utayarishaji wa ramani za majengo. Mamlaka hizo zishauriwe kuwasiliana na vyama vya watu wenye Ulemavu ili kubaini mahitaji muhimu ya watumishi wenye ulemavu.

(c) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitenge maeneo maalum kwa ajili ya kuegesha magari au vyombo vingine vya usafiri vinavyotumiwa na watu wenye ulemavu. Maeneo maegesho yawe karibu na majengo ya ofisi ili

kuwawezesha watu wenye ulemavu kufika kwa urahisi kwenye vyombo vya usafiri.

**Jedwali Na. 3: Masharti kwa Waajiri ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kufika mahali pao pa kazi.**

- Fanya marekebisho ili kuhakikisha kwamba ofisi inayotumiwa na mtumishi mwenye ulemavu inafikika kwa urahisi.
- Fanya marekebisho ya ziada mahali pa kazi ili kumwezesha mtumishi mwenye ulemavu kumudu mazingira ikiwa ni pamoja na marekebisho ya samani, nyenzo na vyoo.
- Weka mteremko wa kushukia na kupandia ili wenye ulemavu ambao wanatumia baiskeli za magurudumu matatu waweze kuzifikia ofisi zao kwa urahisi.
- Teua mtu wa kumsaidia mtumishi asiyeona pindi anapohitaji msaada huo.
- Hakikisha kuwa kuna choo ambacho kinaweza kutumiwa na watumishi wenye ulemavu wa viungo.

## 3.7 Upatikanaji wa Taaarifa na Mawasiliano.

(a) Watu wenye ulemavu na familia zao wana haki ya kupata taarifa kamili juu ya hali zao za afya, huduma na kuingizwa katika programu za ustawi wao. Waajiri watoe taarifa kwa njia ambazo zitawafikia watumishi wenye ulemavu bila matatizo.

(b) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zipange mikakati ya utoaji taarifa na huduma mbalimbali ili kuyafikia kwa urahisi makundi mbalimbali ya watumishi wenye ulemavu. Kwa mfano, mfumo wa maandishi unaotumiwa na wenye ulemavu wasioona, maandishi makubwa na teknolojia nyingine zinapaswa kutumika ili taarifa za maandishi ziweze kuwafikia wasioona. Hali kadhalika, teknolojia kama hiyo itumike kuhakikisha kuwa walemavu wenye tatizo la ufahamu wanapata taarifa ya mdomo.

(c) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kwamba huduma za kutafsiri lugha ya ishara au alama zinapatikana ili kurahisisha mawasiliano kati ya wenye ulemavu wa kusikia na watumishi wengine.

(d) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kwamba taarifa mpya za mifumo ya mawasiliano ya

kompyuta na miundo mingine ya utoaji huduma inayotolewa kwa jamii inawafikia pia watumishi wenye ulemavu.

## 3.8 Usawa wa Kijinsia na Ulemavu.

(a) Wakati wa utoaji wa huduma, Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kwamba mahitaji ya kijinsia kwa wanaume na wanawake yanazingatiwa kikamilifu. Mtumishi mwenye ulemavu asibaguliwe au kunyimwa huduma kwa misingi ya jinsia yake.

(b) Usawa wa Kijinsia na uchanganuzi wa masuala ya kijinsia utasisitizwa na kuzingatiwa na mameneja wote wa utumishi wa umma. Hatua hii itapunguza uwezekano wa wanawake wenye ulemavu kuathirika zaidi na matatizo yanayohusiana na ulemavu.

(c) Mipango na huduma kwa ajili ya wenye ulemavu mahali pa kazi itazingatia masuala ya kijinsia ikiwa ni pamoja na mahitaji maalum ya wanawake wenye ulemavu katika utumishi wa umma.

## 3.9 Kuwalinda wenye Ulemavu dhidi ya Maambukizo ya UKIMWI.

(a) Taarifa juu ya kujikinga na maambukizo ya Virusi vya Ukimwi na kuenea kwa UKIMWI na huduma zingine mahali pa kazi zizingatie mahitaji ya watumishi wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kupata maambukizo ya UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa.

(b) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kwamba taarifa na huduma zinazohusu janga la UKIMWI zinawafikia watumishi wenye ulemavu kwa njia ambayo ni rahisi. Kwa mfano, kuweka katika maandishi ya nukta nundu yanayotumiwa na wasioona au kwa kupitia katika kanda za redio kwa ajili ya wasioona na kusikia. Kwa wale wenye udhaifu wa kujifunza (learning disability), maelezo yanaweza kutolewa kwa mdomo na vitendo.

## 3.10 Huduma za Afya.

Wizara, Idara, Wakala wa Sekarili na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa watu wenye ulemavu wanapata:-

(a) Huduma za afya kwa utaratibu unaotumika kwa watumishi wengine na kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa.

(b) Matibabu ya mara kwa mara kwa kadri ya mahitaji yao ili kulinda na kuboresha utendaji wao. Gharama za matibabu pamoja na gharama za usafiri na fedha za kujikimu zilipwe na waajiri kwa mujibu wa kifungu K cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 1994.

## 3.11 Kuwawezesha Wenye Ulemavu Kuishi Maisha yenye hadhi.

Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali ya Mitaa zihakikishe kuwa fedha kwa ajili ya kutoa huduma za kuwawezesha watumishi wenye ulemavu kuishi maisha yenye hadhi na kuendelea kufanya kazi (Rehabilitation) zinatolewa. Waajiri wote watazingatia yafuatayo:-

(a) Kuandaa mipango inayohusiana na kuwezesha wenye ulemavu kufanya kazi zao kikamilifu. Mipango hiyo itaandaliwa kwa kuzingatia mahitaji binafsi ya watumishi wenye ulemavu na kwa misingi ya usawa na ushirikishwaji.

(b) Kuandaa mipango ya shughuli au kazi mbalimbali. Kwa mfano, mafunzo ya kukuza stadi ili kuboresha utendaji wa kazi, kutoa nasaha kwa watumishi wenye ulemavu na familia zao, kujenga moyo wa kujitegemea na kutoa huduma za mara kwa mara nk.

(c) Kuwahimiza watumishi wenye ulemavu na familia zao kujishughulisha katika kazi za kuwawezesha kuishi maisha yenye hadhi na kuboresha afya zao. Kwa mfano, kushiriki katika michezo mbalimbali, kushiriki katika kazi mbalimbali kama vile kufundisha au utoaji wa ushauri nasaha katika sehemu za kazi au katika jamii.

(d) Wakati wa kuandaa programu za kuwawezesha wenye ulemavu kuishi katika maisha yenye hadhi kwa kufanya kazi za kujitegemea, utaalam kutoka vyama vya wenye ulemavu utumike.

## 3.12 Nyenzo na Vifaa vya kuwaongezea uwezo wenye Ulemavu.

Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kwamba watumishi wenye ulemavu wanapata huduma zitakazowasaidia kutekeleza majukumu yao kimamilifu kama vile nyenzo na vifaa ili kuwasaidia kuongeza kiwango chao cha kujitegemea katika maisha yao ya kila siku:-

(a) Kuwapatia watumishi wenye ulemavu nyenzo na vifaa vya kuwaongezea uwezo kwa kadri ya mahitaji yao.

(b) Kusaidia katika matengenezo, ugawaji na ukarabati wa nyenzo na vifaa vyao na kutoa mafunzo juu ya matumizi na matunzo yake.

(c) Kutambua kuwa ni haki ya watumishi wenye ulemavu kupatiwa mahitaji yao muhimu kama vile vifaa vya kuwaongezea uwezo, fedha kwa ajili ya matibabu na ukarabati wa afya zao (rehabilitation). Nyenzo na vifaa hivi vitolewe na waajiri au vitolewe kwa gharama nafuu ambayo watumishi wenye ulemavu au familia zao wataweza kumudu kununua.

(d) Mahitaji maalum ya wanawake na wanaume kuhusu muundo, ubora na muda wa uchakavu yazingatiwe wakati wa kuandaa mipango ya kuwapatia nyenzo na vifaa vya kuwaongezea uwezo watumishi wenye ulemavu.

**Jedwali Na. 4: Baadhi ya nyenzo na vifaa vinavyoweza kutolewa kwa watumishi wenye Ulemavu ili kuwaongezea uwezo.**

| |
|---|
| ▪ Baiskeli za magurudumu matatu (Tri-motor cycle).<br>▪ Vifaa vya kuongeza usikivu (Hearing Aid).<br>▪ Mashine za maandishi ya nukta nundu kwa wasioona (Braille machines).<br>▪ Karatasi za maandishi ya wasioona (Braille papers).<br>▪ Vitabu vya maandishi ya wasioona (Braille books).<br>▪ Fimbo nyeupe (White canes)<br>▪ Viungo vya bandia (Artificial organs).<br>▪ Mashine maalumu za kupiga chapa.<br>▪ Miwani maalumu. |

## 3.13 Kufanya mabadiliko ya kazi pale inapobidi.

Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweke mazingira ya kuwawezesha watumishi wenye ulemavu kufanya kazi zao kikamilifu na kwa ufanisi. Ili kufanikisha adhima hiyo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

### 3.13.1 Kufanya mabadiliko ya kazi ya muda mfupi.

Mabadiliko ya kazi ya muda mfupi maana yake ni kumpa mtumishi mwenye ulemavu kazi tofauti na aliyokuwa anafanya mwanzo. Kazi hiyo si lazima iwe inahitaji kutumia stadi na ujuzi wa kazi yake ya mwanzo.

(a) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimbadilishie kazi mtumishi mwenye ulemavu kama itaonekana kwamba mtumishi huyo anashindwa kufanya kazi aliyoajiriwa kufanya kwa sababu ya kukithiri kwa ulemavu wake. Utaratibu huu unaleta maana pale mabadiliko ya hali ya ulemavu wa mtumishi husika ni ya muda au hutokea kwa

vipindi. Mabadiliko haya yafanyike baada ya kushauriana kikamilifu na mtumishi husika.

### 3.13.2 Mabadiliko ya Kazi ya Kudumu

(a) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zifanye mabadiliko ya kazi kwa mtumishi mwenye ulemavu anayeomba kurudi kazini baada ya mapumziko yaliyotokana na hali ya ulemavu wake. Mwajiri afanye uchunguzi ili kuona kama mtumishi huyo anaweza kufanya kazi zake kikamilifu. Kila inapowezekana, mtumishi mwenye ulemavu apewe muda wa kuthibitisha uwezo wake wa kufanya kazi aliyoajiriwa mwanzo.

(b) Endapo mtumishi mwenye ulemavu hawezi tena kufanya kazi yake ya awali, na kama kazi anayobadilishiwa anaimudu kwa misingi ya uchambuzi ulioelezwa hapo juu, mwajiri anaweza kufikiria kuyafanya mabadiliko hayo kuwa ya kudumu.

## 3.14 Kupunguza makali ya ulemavu kwa watumishi wenye ulemavu.

(a) Taasisi zote za utumishi wa umma kwa wakati wote zitapaswa kuongeza huduma kwa watumishi wenye ulemavu kwa kuweka mazingira ya afya kwa kuwapa elimu na mahitataji yao mengine muhimu.

(b) Watumishi wenye ulemavu wapewe taarifa na elimu juu ya haki na wajibu wa watumishi kuhusu masuala ya ulemavu, kukuza uwazi juu ya ulemavu na kuwakubali watu wenye ulemavu kama sehemu ya jamii.

(c) Watumishi wenye ulemavu wapewe matibabu kwa kugharamiwa na waajiri kama ilivyo kwa huduma zingine za afya. Mahitaji muhimu kwa watumishi wenye ulemavu yalenge kuongeza ushiriki wao katika shughuli mbalimbali za kijamii.

(d) Menejimenti ya mfumo wa habari na elimu na iliyopo katika Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa iboreshwe na izingatie utoaji wa taarifa juu athari za ulemavu na juu ya hatua zinazofaa kuchukuliwa.

**Jedwali Na. 5: Taarifa itakayopelekwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.**

| |
|---|
| ▪ Idadi ya watumishi wenye ulemavu walioajiriwa kwa mwaka (wanawake na wanaume).<br><br>▪ Idadi ya watumishi wenye ulemavu waliopandishwa vyeo katika taasisi husika (wanawake na wanaume).<br><br>▪ Aina ya vifaa au nyenzo zilizotolewa kwa wenye ulemavu ili kuwaongea uwezo kwa mwaka (wanawake na wanaume).<br><br>▪ Idadi ya watumishi wenye ulemavu waliohudhuria mafunzo kwa mwaka (wanawake na wanaume). |

**3.15 Usafiri na Usalama Barabarani.**

Watumishi wenye ulemavu wanakabiliwa na matatizo makubwa ya usafiri wa kwenda na kurudi kazini. Ili kuhakikisha kuwa watumishi hawa wanatekeleza wajibu wao ipasavyo, Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kwamba:

(a) Pale inaporuhusu, watumishi wenye ulemavu wanapewa usafiri au wenye vyombo vyao vya usafiri kulipiwa gharama za mafuta kwenda na kurudi kazini. Hata hivyo, sharti hili lisitumike kama kigezo cha kumfanya mtumishi mwenye ulemavu kutofika kazini.

(b) Wanashirikiana na wadau wengine wanaojihususha na masuala ya walemavu kuhakikisha kwamba watumishi wenye ulemavu wanapewa vyombo ya kusafiria kama vile baiskeli au pikipiki zenye magurudumu matatu ili kuwaondolea matatizo ya usafiri.

# SURA YA NNE

## WATUMISHI WENYE ULEMAVU NA MABADILIKO YA MENEJIMENTI YA WATUMISHI

### Utangulizi

Ili kuboresha na kuongeza idadi ya watumishi wenye ulemavu katika ajira ya utumishi wa umma, Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zina wajibu wa kuhakikisha kuwa matangazo ya nafasi za kazi yanawafikia pia watu wenye ulemavu. Aidha, watu wenye ulemavu wanaosailiwa na kuonekana wana sifa za kuajiriwa, wapewe nafasi hizo bila kubaguliwa. Ili kuhakikisha kuwa watu wenye walemavu wenye sifa wanapata haki yao ya kuajiriwa, waajiri watazingatia mambo yafuatayo:-

### 4.1 Matangazo ya Kazi.

Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa matangazo ya nafasi za kazi yanayotolewa magazetini yanawafikia watu wenye ulemavu ili waweze kushindania nafasi zinazotangazwa kwa kuzingatia yafuatayo:-.

(a) Katika kueleza sifa ya mwombaji anayefaa kujaza nafasi ya kazi inayotangazwa, waajiri waepuke kuongeza masharti ya ziada ambayo si ya lazima na ambayo yanaweza kuleta hofu kwa waombaji wenye ulemavu.

(b) Waajiri wahakikishe kuwa maelezo yanayotolewa kuhusu ajira yanatoa picha halisi kuhusu mtazamo mzuri wa taasisi kwa watu wenye ulemavu.

(c) Waajiri wahakikishe kuwa matangazo ya kazi katika intaneti yanawafikia pia wenye ulemavu kwa kuweka matangazo hayo katika redio na televisheni.

### 4.2 Usaili/Mahojiano.

Watu wenye ulemavu wanahitaji kuwa katika eneo tulivu wanapofanyiwa usaili au wanapofanya mtihani wa kuomba kazi.

(a) Watu wenye ulemavu wanapoalikwa kwenye usaili, ni vyema kufanya mipango mizuri ya maandalizi. Kwa mfano, kuwa na mtu wa kutafsiri lugha ya ishara ili awasiliane na wasailiwa wenye ulemavu wa kuzungumza.

(b) Wakati wa kumsaili mwombaji asiyeona ni muhimu kuhakikisha kuwa chumba cha usaili kinakuwa na mwanga wa kutosha.

(c) Pale inapowezekana, Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zifanye mashauriano na wasailiwa ili kuhakikisha kuwa mahitaji yao binafsi yanapatikana/yanazingatiwa kabla ya usaili.

(d) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa mahali pa usaili panafikika kwa urahisi kwa wasailiwa wenye ulemavu.

(e) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa wasailiwa wenye ulemavu wana haki sawa na wasailiwa wasio na ulemavu. Wizara, Idara na Wakala wa Serikali ziwape msaada unaohitajika wenye ulemavu ili usaili uwe wa ufanisi.

(f) Wakati wa usaili Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zichambue uwezo wa wasailiwa bila ya kuangalia ulemavu wao. Aidha, Waajiri wajadiliane kwa kina na watumishi wenye ulemavu jinsi ulemavu wao utakavyoathiri utendaji wa kazi zao.

**4.3 Mafunzo.**

Kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 Kifungu cha 103 (1), kila mwajiri ana wajibu wa kutoa mafunzo na kuwaendeleza watumishi wake ikiwa ni pamoja na watumishi wenye ulemavu.

(a) Kila mwajiri, kwa misingi ya maelezo ya kazi, afanye ukaguzi, kutathmini utendaji wa watumishi na kupanga mipango ya maendeleo ya watumishi kwa kuzingatia masharti maalum ya watumishi wenye ulemavu.

(b) Kila mwajiri apange bajeti ya mafunzo kila mwaka kwa ajili ya watumishi wenye ulemavu.

(c) Kwa mujibu kifungu cha 5 (18) cha Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999, kwa lengo la kukuza na kuendeleza stadi za wafanyakazi wote mahali pa kazi, Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziandae

programu za mafunzo na kuwaendeleza watumishi kwa kuzingatia mahitaji ya stadi zilizobainishwa katika mipango ya watumishi.

(d) Maudhui ya programu za mafunzo na maendeleo ya watumishi wenye ulemavu yatajumuisha mafunzo ya vitendo, kupandisha watumishi vyeo, mafunzo ya ufundi, kitaalamu, menejimenti na uongozi.

(e) Kwa kushauriana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaandaa programu za mafunzo kazini kwa ajili ya watumishi wenye ulemavu kwa lengo la kushughulikia masuala yanayohusu haki na wajibu wao.

(f) Licha ya vikwazo vya bajeti, Wizara, Idara, Mawakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kwamba kipaumbele kinatolewa kwa watumishi wenye ulemavu wakati wa kutoa huduma na nafasi mbalimbali za mafunzo.

(g) Wizara ya Elimu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ihakikishe kwamba watu wenye ulemavu wenye sifa na wanaopata udahili katika vyuo vikuu wanapewa mikopo ya masomo bila kujali masharti ya kupata daraja la kwanza katika mitihani yao ya kidato cha sita, vyuoni au kuangalia aina ya kozi wanazotarajia kusoma. Aidha, zoezi la 'upgrading' linalofanyika katika vyuo vikuu liwahusishe pia watu wenye ulemavu ili waweze kufikia viwango vya udahili.

### 4.4 Malalamiko na Taratibu za Kinidhamu.

Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zifuatilie malalamiko yanayotolewa na watumishi wenye ulemavu au wawakilishi wao bila kuchelewa. Waajiri wachukue hatua za kinidhamu dhidi ya mtumishi ambaye, kwa sababu yoyote, atawabagua watumishi wenye ulemavu kwa misingi ya ulemavu wao.

### 4.5 Masharti ya Kazi.

(a) Watumishi wenye ulemavu watatawaliwa na masharti ya kazi sawa na watumishi wasio walemavu.

(b) Wakati wa kurekebisha Sera na Kanuni za Utumishi wa Umma, waajiri wahakikishe kwamba watumishi wenye ulemavu wanaendelea kupata haki zao za kiutumishi kama watumishi wasio walemavu.

### 4.6 Kushughulikia Kazi ya Ziada.

Waajiri watabuni utaratibu wa kushughulikia kazi ya ziada pale inapotokea kwamba mtumishi mwenye ulemavu, kutokana na ulemavu wake, ameondoka mahali pa kazi kwa ajili ya matibabu. Hata hivyo, muda wa kukosa kufika kazini kwa ajili ya matibabu hautazidi ule unaokubalika katika Kanuni za Serikali.

### 4.7 Likizo ya Ugonjwa.

(a) Mtumishi mwenye ulemavu ana haki ya kupata likizo ya ugonjwa yenye masharti sawa na ya watumishi wasio walemavu wanapokuwa wagonjwa kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

**(b)** Watumishi wenye ulemavu wanaweza kuomba likizo kwa ajili ya matibabu au likizo ya ugonjwa kama ilivyoelezwa katika kifungu cha K. 19 cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 1994.

## SURA YA TANO

## KUANDAA MIPANGO NA BAJETI KWA AJILI YA WATUMISHI WENYE ULEMAVU

### Utangulizi

Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziandae mipango madhubuti itakayoziwezesha kujua mambo ya kutekelezwa ili kufikia malengo waliyojiwekea katika utoaji wa huduma kwa kutumia fedha na rasilimali zilizopo. Iandaliwe mipango ya muda mrefu pamoja na mipango ya uendeshaji ambayo itaonyesha malengo maalum ya muda mfupi kwa ajili ya ustawi wa watumishi wenye ulemavu.

**Jedwali Na. 6: Masuala Muhimu ya Kuzingatia Kuhusu Watumishi wenye Ulemavu**

| |
|---|
| ▪ Tambua idadi ya watumishi wenye ulemavu mahali pa kazi.<br><br>▪ Unganisha elimu na taarifa za wenye ulemavu katika programu za mafunzo na fanya tathmini ya programu hizo.<br><br>▪ Tambua nyenzo na zana wanazohitaji watumishi wenye ulemavu kisha panga namna ya upatikanaji wake.<br><br>▪ Tenga fedha na rasilimali ya kutosha kwa ajili ya mipango, vifaa na nyenzo za kuwaongezea uwezo kwa watumishi wenye ulemavu. |

## 5.1 Hatua za Kufuata Kabla ya Kuanza Kuandaa Mipango.

Kabla ya kuanza kuandaa mipango kwa ajili ya watumishi wenye ulemavu, Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziangalie mambo yanayopewa kipaumbele na serikali kuhusu masuala ya kijamii na kiuchumi pamoja na mpango wa muda wa matumizi ya serikali. Hatua hii itazisaidia Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kubuni na kuingiza vipaumbele hivyo katika mipango mkakati ya sekta zao.

## 5.2 Kukusanya taarifa kwa ajili ya kuandaa Mipango

(a) Ili kupata taarifa sahihi kwa ajili ya kuandaa mipango, kila Wizara, Idara na Wakala wa Serikali zifanye uchambuzi wa hali halisi ili kutambua mambo yanayochangia hali ya hatari na uwezekano wa kuathirika kwa watumishi wenye ulemavu mahali pa kazi.

(b) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitapaswa kutambua mazingira ya kazi ambayo yanaweza kusababisha watumishi wenye ulemavu kutofika kazini. Upangaji wa mipango uzingatie na kushughulikia pia masuala yanayohusiana na ongezeko la kazi kutokana na watumishi wenye ulemavu kutofika kazini. Mifumo mipya ya kiutumishi kama vile mtumishi kuwa na stadi nyingi ni muhimu izingatiwe ili kuongeza ufanisi.

**Jedwali Na. 7: Masuala Muhimu ya Kuzingatia wakati wa kuandaa Mipango kwa ajili ya Wenye Ulemavu.**

| |
|---|
| ▪ Ni yapi malengo ya Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa watumishi wenye ulemavu?<br>▪ Kuna uhusiano wowote wa kiwango cha juu kati ya malengo ya serikali juu ya ulemavu na yale ya Wizara, Idara,Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa?<br>▪ Je malengo ya kimkakati na matokeo ya Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa yanahusiana na majukumu muhimu katika mamlaka hizo?<br>▪ Ni zipi athari za sasa na za baadaye za ulemavu kwa Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa?<br>▪ Kwa jinsi gani athari za ulemavu zitaathiri malengo ya jumla ya Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa?<br>▪ Matokeo ya mipango ya ulemavu ambayo imeandaliwa ni ya manufaa kwa walemavu?<br>▪ Malengo na maazimo yamefikiwa?<br>▪ Ni rasilimali gani (ya fedha au watumishi) zinahitajika kwa utekelezaji wa mipango ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kwa ajili ya walemavu? |

## 5.3 Kupanga Bajeti

Utoaji wa nyenzo na vifaa vya kuwaongezea uwezo wenye ulemavu, huduma za kufasiri lugha za alama na ishara ni muhimu ili kuhakikisha kwamba watumishi wenye ulemavu wanashiriki kikamilifu katika Utumishi wa Umma. Ukosefu au ufinyu wa bajeti kwa ajili ya utoaji wa huduma hizi kwa watumishi wenye ulemavu ni kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa mipango ya ustawi wao. Kwa hiyo Wizara, Idara, Wakala wa serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa:-

(a) Zihakikisha kwamba fedha za kutosha zinatengwa katika bajeti zao ili kununua nyenzo na vifaa vya bei nafuu pamoja na huduma mbalimbali kwa watumishi wenye ulemavu.

(b) Zishirikiane na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali, wabia wao, wafadhili na wakala wa maendeleo ambao wanatoa matibabu, vifaa na nyenzo na wanaopanga mipango ya kuwawezesha walemavu kuendesha miradi yao ya kujitegemea ili waweze kuishi

maisha ya kawaida au waweze kupata vifaa na huduma wanazohitaji kwa bei nafuu.

(c) Zihakikishe kwamba gharama halisi zinazohitajika kwa ajili ya mipango ya kimkakati ambayo inajumuisha pia masuala ya watumishi wenye ulemavu, zinaingizwa katika makadirio ya bajeti ya muda wa kati. Hatua hii itawezesha Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa bajeti halisi kabla ya kuwasilisha Wizara ya Fedha.

## SURA YA SITA

## HAKI NA WAJIBU WA WAAJIRI NA WATUMISHI WENYE ULEMAVU

### Utangulizi

Upatikanaji wa taarifa juu ya nyaraka za utumishi wa umma na huduma kwa watumishi wenye ulemavu ni muhimu sana kwao, na ni sehemu ya kuwapatia huduma wanayohitaji. Kwa hivi sasa, watumishi wenye ulemavu wanakosa njia ya kupata taarifa wanazohitaji kwa ustawi wao. Waajiri na watumishi wa umma wenye ulemavu wana haki na wajibu katika kufanikisha adhima hii.

(a) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kwamba nyaraka za utumishi wa umma kama vile Sheria, Sera, Kanuni, n.k. zinasambazwa kwa watumishi wenye ulemavu kwa kutumia miundo unaofaa. Kwa mfano, kwa maandishi makubwa, maandishi kwa ajili ya wasioona, kwa redio, televisheni, intaneti nk.

(b) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitenge fedha za kutosha katika bajeti zao kwa ajili ya ununuzi wa zana na vifaa maalumu na teknolojia ya kuwawezesha watumishi wenye ulemavu kupata taarifa kwa urahisi.

(c) Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zianzishe mfumo wa kumbukumbu katika kompyuta ambazo zinahusiana na watumishi wenye ulemavu ili kusaidia na kuboresha utoaji wa taarifa. Taarifa hizi ziwasilishwe Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kila zinapohitajika.

## 6.1 Waajiri Katika Utumishi wa Umma.

Zifuatazo ni haki na majukumu ya waajiri kuhusu masuala ya watu wenye walemavu:

(a) Kukubali ombi la mtumishi mwenye ulemavu la kupewa mahitaji ya kiufundi isipokuwa kama kuna sababu maalumu itakayomfanya kukataa ombi hilo.

(b) Kupata ushauri kutoka wataalamu wa afya juu ya watumishi wenye ulemavu pale inapohitajika.

(c) Kuhakikisha kwamba kumbukumbu za maombi yote yanayotoka kwa watumishi wenye ulemavu na hatua zilizochukuliwa zinahifadhiwa vizuri katika jalada la mtumishi husika.

(d) Kudumisha utunzaji wa siri wa taarifa za matibabu za mtumishi mwenye ulemavu.

## 6.2 Watumishi wenye ulemavu.

Zifuatazo ni haki na wajibu kwa watumishi wenye ulemavu:

(a) Kutoa taarifa kwa mwajiri wake juu ya hali yake ya ulemavu.

(b) Kuweka wazi (kwa maandishi) kuhusu mahitaji yake na masharti ya afya au ulemavu wake kutoka kwa wataalamu wa afya, ili mwajiri aweze kushughulikia ipasavyo mahitaji hayo.

(c) Kuwa mwanachama wa chama chochote cha watu wenye ulemavu ili kumwezesha kuwa na sauti katika kuomba mahitaji yake kutoka serikalini.

(d) Kutekeleza wajibu wake wa kazi kwa kiwango kilichokubaliwa baada ya kutekelezewa mahitaji yake.

(e) Kutoa ushirikiano kwa mwajiri wake ili aweze kutekelezewa mahitaji yake ya kiufundi.

(f) Kujadili masuala ya ulemavu wake na Maafisa waliopewa mamlaka ya kushughulikia masuala ya walemavu tu. Hawa ni pamoja na msimamizi wake wa kazi, mwakilishi wa chama cha walemavu na afisa wa haki za binadamu.